

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA**



MKUTANO WA NNE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA SITA

MKUTANO WA NNE

YATOKANAYO NA KIKAO CHA SITA - TAREHE 14 SEPTEMBA, 2016

I. DUA:

Saa 3.00 asubuhi Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mwenyekiti wa Bunge ilisoma Dua na kuliongoza Bunge.

MAKATIBU MEZANI:

1. Ndg. Ruhilabake Theonest
2. Ndg. Charles Mloka
3. Ndg. Asia Ninja

II. MASWALI:

Maswali yafuatayo yaliulizwa:-

1. OFISI YA WAZIRI MKUU:

Swali Na. 71 : Mhe. Boniventura Destery Kiswaga
Nyongeza: i) Mhe. Boniventura Destery Kiswaga
ii) Mhe. George Malima Lubeleje
iii) Mhe. John John Mnyika

2. OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Swali Na. 72 : Mhe. Ester Lukago Midimu
Nyongeza: i) Mhe. Ester Lukago Midimu
ii) Mhe. Joseph Roman Selasini
iii) Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq

3. OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA NA MUUNGANO):

Swali Na. 73: Mhe. Joseph George Kakunda (liliulizwa na Mhe. Albert Ntabaliba Obama)
Nyongeza: Mhe. Albert Ntabaliba Obama.

4. WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

Swali Na. 74 :Mhe. Susan Limbweni Kiwanga
Nyongeza: i) Mhe. Susan Limbweni Kiwanga
ii) Mhe. Venance Mwamoto

5. WIZARA YA KILIMO NA MIFUGO:

Swali Na. 75 :Mhe. Joram Ismael Hongoli
Nyongeza: i) Mhe. Joram Ismael Hongoli
ii) Mhe. Pauline Gekul

6. WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

Swali Na. 76 :Mhe. Rashid Ali Abdallah

- Nyongeza: i) Mhe. Rashid Ali Abdallah
ii) Mhe. Catherine Valentine Magige
iii) Mhe. Savelina Silvanus Mwijage

Swali Na. 77 : Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel

- Nyongeza: i) Mhe. Dkt. Godwin Oloyce Mollel
ii) Mhe. Juma Selemani Nkamia
iii) Mhe. Maryam Salum Msabaha

7. WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

Swali Na. 78: Mhe. Abdallah Khamis Ulega (liliulizwa na Mhe. Mbaraka Kitwana Dau)

Nyongeza: Mhe. Mbaraka Kitwana Dau.

Swali Na. 79: Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa

Nyongeza: Mhe. Mohamed Omary Mchengerwa.

8. WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:

Swali Na. 80: Mhe. John Wegesa Heche (liliulizwa na Mhe. Joseph Michael Mkundi)

Nyongeza: Mhe. Joseph Michael Mkundi.

Swali Na. 81: Mhe. Subira Khamis Mgusu

Nyongeza: Mhe. Subira Khamis Mgusu.

9. WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:

Swali Na. 82: Mhe. Zainab A. Katimba aliuliza pamoja na maswali ya nyongeza.

Swali Na. 83: Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi

Nyongeza: Mhe. Zainab Nuhu Mwamwindi.

10. WIZARA YA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI:

Swali Na. 84: Mhe. John Peter Kadutu (liliulizwa na Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka)

Nyongeza: Mhe. Emmanuel Adamson Mwakasaka.

Swali Na. 85: Mhe. Yahaya Omar Massare

Nyongeza: Mhe. Yahaya Omar Massare.

III. MATANGAZO:

1. Mwenyekiti alitoa pongezi kwa Waziri Mkuu kwa Harambee ya kusaidia wahanga wa tetemeko Bukoba. Pia aliwapongeza Wabunge kwa kutoa posho yao ya siku moja kwa ajili hiyo.
2. Wageni mbalimbali waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na kuona namna Bunge letu linavyofanya kazi walitambulishwa wakiwemo Wabunge Saba (7) kutoka nchini Kenya.

IV. MWONGOZO WA SPIKA:

1. Mhe. Joseph Roman Selasini alitumia Kanuni ya 68 (7) kuhusu tuhuma zilizoandikwa na Gazeti la Nipashe kwamba Wabunge wametuhumiwa kwa rushwa zilizotolewa na Mhe. Seif Khamis Gulamali akisema tuhuma hizo zinaingilia haki za Wabunge hivyo ni vema Mbunge husika atoe maelezo na awataje wahusika. Mwenyekiti alitoa maelezo kwamba Bunge halifanyi kazi na vyombo vyaa habari.
2. Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara na Mhe. Pascal Yohana Haonga walitumia Kanuni ya 68(7) wakihoji kutotambuliwa kwa Kiongozi wa Upinzani na Mwenyekiti wakati akitoa salamu za shukrani kwa walioenda Bukoba kusaidia Wahanga wa tetemeko na kumtaja Waziri Mkuu pekee. Mwenyekiti aliomba radhi kwa hilo na kumtambua Kiongozi wa Upinzani na kusisitiza jambo hili si vema likawagawa Wabunge ni la Taifa zima.

V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi aliwasilisha Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo wa 2016 (*The Tanzania Agricultural Research Institute Bill, 2016*);

Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu aliwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu Muswada tajwa hapo juu;

Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi aliwasilisha Maoni ya Upinzani juu ya Muswada tajwa hapo juu;

Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi aliwasilisha Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi wa Mwaka 2016 (*The Tanzania Fisheries Research Institute Bill, 2016*);

Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma aliwasilisha Maoni ya Kamati kuhusu Muswada tajwa hapo juu;

Mhe. Dkt. Sware Semesi aliwasilisha Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada tajwa hapo juu.

MWONGOZO WA SPIKA:

Mhe. John John Mnyika aliomba kupatiwa Jedwali la Marekebisho la Serikali ili kusaidia Wabunge kuchangia. Kiti kilielekeza zinaandaliwa na Wabunge watapatiwa.

Mjadala wa jumla wa Miswada yote miwili ulianza kama ifuatavyo:-

- | | | |
|---------------------------------|---|-----|
| 1) Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki | - | CCM |
| 2) Mhe. Salum Mwinyi Rehani | - | CCM |

VI. KUSITISHA BUNGE:

Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni.

VII. BUNGE KUREJEA:

Bunge lilirejea Saa 11.00 Jioni lilirejea, na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mwenyekiti aliendelea kukiongoza Kikao na mjadala kwa Miswada ya Sheria ya Serikali uliendelea:-

- | | | |
|---------------------------------------|---|---------|
| 3) Mhe. Zuberi Mohammed Kuchauka | - | CUF |
| 4) Mhe. Pascal Yohana Haonga | - | CHADEMA |
| 5) Mhe. Dkt. Christine Ishengoma | - | CCM |
| 6) Mhe. Richard Philip Mbogo | - | CCM |
| 7) Mhe. Jitu Vrajlal Soni | - | CCM |
| 8) Mhe. Fatma Hassan Tawfiq | - | CCM |
| 9) Mhe. Cecilia Daniel Paresso | - | CHADEMA |
| 10) Mhe. Mwita Mwikwabe Waitara | - | CHADEMA |
| 11) Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya | - | CUF |
| 12) Mhe. Ester Michael Mmasi | - | CCM |
| 13) Mhe. Joseph George Kakunda | - | CCM |
| 14) Mhe. Flatei Gregory Masay | - | CCM |
| 15) Mhe. Japhet Ngailonga Hasunga | - | CCM |
| 16) Mhe. Jacquiline Ngonyani Msongozi | - | CCM |
| 17) Mhe. Riziki Said Mngwali | - | CUF |
| 18) Mhe. Peter Ambrose Lijualikali | - | CHADEMA |

TAARIFA:

Mhe. Goodluck Asaph Mlinga alimpa taarifa Mhe. Peter Lijualikali kuwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Dodoma ameteuliwa kwa sifa zake (LLM) na siyo kutokana na kuwa na Kadi ya CCM. Taarifa hiyo ilikataliwa na Mhe. Lijualikali.

- | | | |
|--------------------------------|---|---------|
| 19) Mhe. David Ernest Silinde | - | CHADEMA |
| 20) Mhe. Abdallah Khamis Ulega | - | CCM |

VIII. BUNGE KUREJEA:

Bunge lilirejea na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto alitoa Taarifa na Bunge lilihojiwa. Muswada ulisomwa kwa Mara ya Tatu na kupitishwa.

IX. KAMATI YA BUNGE ZIMA:

Bunge lilikaa tena kama Kamati ya Bunge Zima kwa ajili ya kupitisha ibara kwa ibara Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Wanataaluma wa Kemia wa Mwaka 2016 (*The Chemist Professionals Bill, 2016*) na kuupitisha. Bunge lilirejea na baada ya kupata Taarifa Wabunge walihojiwa na kupitisha Muswada huo.

X. KUAHIRISHA SHUGHULI ZA BUNGE:

Saa 1.45 usiku Bunge lilahirishwa hadi tarehe 15/09/2016 Saa 3.00 Asubuhi.

DODOMA
14 SEPTEMBA, 2016

DKT. T. D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE